

SKPS mabadiliko ya kuvaa barakoa kuanzia mwanzoni wa Julai 1, 2021 SKPS Familia

Idara ya Elimu ya Oregon kwa sasa inaruhusu wilaya za shule kufanya mabadiliko ya itifaki ya afya na usalama kwa kushirikiana na mamlaka za afya ya umma. Kwa mwongozo wa hivi karibuni mamlaka ya afya ya Oregon (OHA) na Idara ya Elimu ya Oregon (ODE) wanashauri barakoa kwa wanafunzi wote kuanzia chekechea mpaka juu na wafanyakazi wote wakati wanafunzi wakiwa ndani ya majengo. Kwawale wenye matatizo ya kiafya au ulemavu wanaweza kupewa uangalizi tofauti. Kwa kuongezea tumekuwa kutikutana na mamlaka za afya ya Marion na Polk kuzungumzia mwongozo wa wanafunzi na watu wazima na tutaendelea kuangalia kwa karibu mwongozo kama unavyotolewa hapo chini na kufanya mabadiliko kama yanatakiwa.

Wilaya ya shule inampango wa kufundisha uso kwa uso kwa siku tano ndani ya wiki kuanzia Septemba. Tunamatumaini kwamba mwongozo ufuatao utatuweka mahali ambapo wanafunzi na wafanyakazi wa shule wataweza kurudi shuleni bila ya haja ya kuvaa barakoa tunapoanza fall.

Mabadiliko ya mara moja kufuatia mwongozo wetu kuanzia Julai 1, 2021 ni kama yafuatayo:

- Wanafunzi watatakiwa kuvaa barakoa ndani na kwenye basi la shule mpaka watakapojulishwa.
- Wafanyakazi wanatakiwa kuvaa barakoa wanapokuwa ndani na wanapokuwa karibu na wanafunzi. Hii inamaanisha pia wanapokuwa kwenye basi la shule. Kuwa karibu inamaanisha ndani ya umbali wafuti tatu wa mwanafunzi kwa dakika 15 au zaidi.
- Wafanyakazi na wanafunzi siyo lazima kuvaa barakoa wanapokuwa nje.
- Mtu yeyote anaweza kuchagua kuvaa barakoa hata pale pasipohitajika kuvaa.
- Umbali wa kimwili utaendelea ndani ya majengo walau umbali wa futi tatu ikiwezekana.

Familia zitapokea taarifa zaidi wakati wa kurudi mashuleni mara zitakapotokea.